

Afya ya Akili Kimataifa

Ombi la Pendekezo la Mradi

Programu ya Afya ya Akili Kimataifa ya Grand Challenges Canada inaunga mkono Mawazo ya Kijasiri yenye Matokeo Chanya.® Lengo la programu hii ni kuzipatia mtaji (seed) na kuzipanua (transition to scale) vumbuzi zenye matokeo chanya zinazoshughulikia mahitaji ya afya ya akili ya watu wasiopata huduma za kutosha, hasa vijana, katika nchi za kipato cha chini na kati.

Afya ya Akili ya Vijana

Changamoto za afya ya akili zinachangia asilimia 14 ya mzigo wa ugonjwa huu ulimwenguni kote; huku asilimia 81 ya mzigo huu ikiwa katika nchi za kipato cha chini na kati. Mzigo wa afya ya akili kimataifa unaongezeka zaidi kwa vijana kutokana na kukosa ufikio wa huduma zilizo rafiki kwa vijana. Afua za awali kwa vijana ni muhimu ili kuwapa vijana hawa usaidizi na stadi za kusaidia kutokomeza mzigo wa afya ya akili unaonekana katika utu uzima.

Ruzuku ya mtaji inayofikia CAD \$250,000 inapatikana ili kuziandaa na kuzijaribu vumbuzi kwa zaidi ya miezi 18 au 24 ambazo zinakidhi mahitaji ya afya ya akili ya watu wasiopata zaidi huduma za kutosha wenye miaka 10 hadi 24 katika nchi za kipato cha chini na kati. Mbinu husika zinahitaji kuongeza uelewa wa afya ya akili na/au kutoa huduma zilizo rafiki kwa vijana.

Vijana na vijana wenye uzoefu halisi wa changamoto za afya ya akili wanapaswa kuhusishwa tangu mwanzo. Tunategemea vumbuzi zote zizingatie utamaduni, zisimamiwe na makundi ya jumuiya, na zitumie mbinu inayoweka kipaumbele kwa mtu na kujikita katika taratibu za haki kuhusiana na afya ya akili.

Matokeo yanayopewa Kipaumbele

Vumbuzi zinapaswa angalau kuleta mojawapo ya matokeo yafuatayo yanayopewa kipaumbele:

- Kuboresha utendaji
- Kuboresha ustawi
- Kupunguza ukali wa dalili
- Kuongeza ustahimilivu

Tunavutiwa hasa na vumbuzi ambazo:



Zinatumia miundo ya wanarika kwa wanarika

Zinashughulikia imani potofu kuhusu jinsia na mahitaji ya afya ya akili ya watu wenye utambulisho tofauti wa kingono na kijinsia.



Zinatoa huduma kupitia michakato iliyo rafiki kwa vijana na isiyo ya utoaji wa kawaida wa huduma za afya

Zinaunganisha afua za afya ya akili na/au ustawi kwenye mifumo iliyopo ya elimu au huduma za kijamii



Zinazotumia teknolojia inayotumiwa na kuaminiwa sana

Programu ya Afya ya Akili Kimataifa inashirikiana na Idara ya Afya na Huduma za Kijamii ya Uingereza kwa kutumia UK Aid kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya na Masuala ya Kimataifa Canada.

Miradi inapaswa kuwa ya kimageuzi, inayolenga kubadili mitazamo kuhusiana na afya ya akili, na inayotolewa kupitia taratibu zilizo sahihi kitamaduni kwa kufanya kazi na vijana wenye uzoefu halisi, kuendeleza mifumo mahalia, na ikiwezekana kushirikisha serikali za mitaa na watunga sera.

Mashirika yanayoongozwa na vijana yatapelewa kipaumbele. Hii inajumuisha mashirika ambayo asilimia hamsini (50%) au zaidi ya watu wenye nafasi muhimu ni vijana wenye miaka 35 kushuka chini.

Vigezo vya Ustahiki

Waombaji stahiki wanajumuisha makampuni ya kijamii na mashirika yanayotambulika kisheria (k.m., yasiyo ya kupata faida, ya kupata faida, makampuni binafsi, taasisi za utafiti/taaluma) ambao:

- Wamesajiliwa kisheria katika nchi zenye ustahili zilizoordheshwa katika Nyongeza A ya Ombi la Pendekezo la Mradi na /au Canada. (Tafadhali zingatia: Waombaji wa Canada lazima watekeleze mradi wao katika nchi stahiki zilizoordheshwa katika Nyongeza A ya Ombi la Pendekezo la Mradi)
- Wanaweza kutekeleza kikamilifu shughuli katika eneo lao la kiufundi
- Wanaweza kupokea na kusimamia fedha za ruzuku

Tarehe Muhimu

Novemba 23, 2021 saa 12:00 pm EST (5:00pm UTC) – Mwisho wa Kusajili Akaunti ya Fluxx. Waombaji wote LAZIMA wasajili akaunti kwenye tovuti ya Grand Challenges Canada Fluxx Portal ifikapo tarehe hii. Usajili wa akaunti utakaofanyika baada ya tarehe na muda huu hautashughulikiwa. Waombaji waliojisajili kufikia tarehe hii ndiyo TU watakaoweza kuwasilisha maombi.

Desemba 1, 2021 saa 12:00pm EST (5:00pm UTC) – Mwisho wa Kuwasilisha Maombi. Waombaji wote LAZIMA wawasilishe maombi kupitia tovuti ya Grand Challenges Canada Fluxx Portal ifikapo tarehe hii ili wazingatiwe kwa ajili ya ufadhili.



Kwa taarifa zaidi kuhusu programu ya Afya ya Akili Kimataifa na fursa ya kupata ufadhili, tafadhali tembelea <https://www.grandchallenges.ca/programs/global-mental-health/>

Tafadhali tuma maswali kuhusu Ombi la Pendekezo la Mradi ambayo hayapo kwenye Maswali Yanayoulizwa Mara Kwa Mara kwenda globalmentalhealth@grandchallenges.ca

Programu ya Afya ya Akili Kimataifa inashirikiana na Idara ya Afya na Huduma za Kijamii ya Uingereza kwa kutumia UK Aid kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Afya na Masuala ya Kimataifa Canada.